









Ni Wakati Gani Ninapaswa Kusalia Nyumbani?

NINAHISI JOTO JINGI MWILINI	NINATAPIKA	NINAHARISHA	NINA UPELE	NINA KIKOHOZI AU NINATATIZIKA KUPUMUA	NINA MAAMBUKIZI KWENYE JICHO	NIMEKUWA HOSPITALINI	SIWEZI KUONJA AU KUNUSA
							
Halijoto ya 100° F au zaidi	Ndani ya saa 24 zilizopita	Ndani ya saa 24 zilizopita	Upele wa mwili unaotokwa na majimaji au ulio na joto jingi	USICHELEWE Kwenda matibabu ikiwa unatatizika kupumua	Wekundu, mwasho, na/au usaha kutoka jichoni	Kukaa hospitalini na/au kutembelea chumba cha dharura	Ndani ya saa 24 zilizopita

Niko tayari kurudi shuleni nitakapokuwa...

Sina joto jingi mwilini bila kutumia dawa kwa saa 24 (yaani, Tylenol, Motrin, Advil).	Sijatapika kwa saa 24.	Sijaharisha kwa saa 24.	Sina upele au joto jingi na nimefanyiwa uchunguzi na mtoa huduma wangu wa afya ikihitajika.	Nimefanyiwa uchunguzi na mtoa huduma wangu wa afya ikihitajika.	Sitokwi na makamasi na/au nimefanyiwa uchunguzi na mtoa huduma wangu wa afya ikihitajika.	Nimeruhusiwa na mtoa huduma wangu wa afya kurejea shuleni.	Nimefanyiwa kipimo cha COVID. Nimepata ushauri wa mtoa huduma wangu wa afya kabla ya kurejea shuleni.
---	------------------------	-------------------------	---	---	---	--	---

Ikiwa mtoto wako ana maumivu kwenye koo au maambukizi mengine ya bakteria, anapaswa kukaa nyumbani hadi awe ametumia dawa ya antibiotiki kwa angalau saa 24 na mtoa huduma wako wa afya awe amemruhusu kurejea shuleni. Tunakuhimiza utafute huduma za matibabu mtoto wako anapokuwa mgonjwa na ufuate mapendekezo ya mtoa huduma wako wa afya kuhusu kurejea shuleni na shughuli nyinginezo.